

- Usafi wa kilimo; vifaa vyovyote viwavyo kutumia kuchuma matawi visafishwe ipasavyo katikati ya 'stools' za ndizi.
- Mimea yenye uwezo wa kustahimili; tumia aina za mbegu zilizo na uwezo wa kustahimili maradhi katika sehemu zinazotahizwa na maradhi ya panama.

Aina za 'apple' ndizi za 'apple' zinazostahimili maradhi

Baadhi ya aina zinazostahimili maradhi ni:

- GT
- Prata-Manyatta Soth, Exera na Kifutu Mysore.

Ng'oa mimea yote ya 'sukari ndizi' ilivyoathiriwa na maradhi ya panama na uibadilishe na aina zinazostahimili zilizotajwa hapo awali. Hakuna tofauti ya utamu kati ya ndizi za GT "apple" linalopendwa zaidi.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Onyango, M

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kisii

S.L.P. 523, KISII,

Simu: (058)31800/1/2/3 au (058)31800


Baruapepe: kari-kisii@westernnet.co.ke

Kisii-kari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 67 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Kukuza ndizi zinazostahimili ugonjwa wa panama



Utangulizi

Fusarium wilt au maradhi ya Panama ni shida sugu katika ukuzaji wa ndizi mikoani Nyanza, Magharibi, Kati, Mashariki na Pwani ya Kenya.

Ugonjwa huu huathiri sana ndizi za aina ya "apple" zijulikanazo sana kama 'sukari ndizi' lakini aina zingine huathiriwa pia kama vile *Gros Michel* au Bogoya, Bokoko na *Silk* japo kwa kiwango kidogo.

Ugonjwa huu unaweza kuangamiza shamba zima la mimea ambayo imeathirika.

Vijidudu vinavyoambukiza ugonjwa huu na jinsi unavyosambazwa

Ugonjwa huu huletwa na aina maaluu ya kuvu ambazo hukua vyema mchangani na kwenye miti inayooza. Ugonjwa huu huingia kwenye mizizi ya miti kupitia pande zilizopasuka.

Halafu unaenea kwenye mti wote kupitia kiwili chake na kukua.

Ugonjwa huu unaweza kuenea kwa kasi katika mimea wote na japo mimea-chipukizi huenda ikaonekana yenye afya huenda ikawa imeathiriwa.

Ishara za maradhi

Mimea ambayo imeathiriwa na panama hutambulika kwa majani kupata rangi ya manjano. Ukianza na majani yale makuu. Baadhi ya majani yatadhoofika, yawe na rangi ya hudhurungi, kisha yafe. Majani mengine hukaa imara lakini punde yanakuwa manjano, hudhurungi, kisha kufa.

Katika hali zingine, pande za nje za jani na za undani hupasuka kutoka juu hadi chini karibu na kuliko mchanga.



Mpasuko wa mihili wa ndizi

Mmea ulioathiriwa hauwezi kukua vyema ili kukuza matunda yaliyokomaa na ugonjwa huwa unaweza kusababisha kufa kwa mimea kabisa, kama picha inavyoonyesha.



Tira ndogo la ndizi zilizokomaa kwenye mmea ulioathirika

Mbinu za kinga

Mbinu za kuinga ugonjwa wa panama ni kama vile:

- Kutosambaa kwa mimea ulioathiriwa hakikisha kwamba mimea ulioathiriwa haujang'olewa kutoka ulipo na kupandwa kwenye sehemu zingine.
- Kinga za kiasili; choma au uzike mimea yote iliyoathiriwa. Badilisha mimea kila mara ndiposa wadudu wafe.